# DINI YA KIISLAMU

## 1.0 UTANGULIZI

Muundo wa mtihani huu umetayarishwa kuwaongoza watahini jinsi ya kutunga maswali ya mtihani. Muundo huu unajumuisha mada zilizomo katika muhtasari (2022) kuanzia Darasa la V, VI na VII. Malengo ya jumla, ujuzi na maudhui ya mtihani yaliyomo humo yanatokana na muhtasari wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu uliotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA-2022) Zanzibar.

## 2.0 MATOKEO YA JUMLA

Baada ya kusoma smo la Dini ya Kiislamu katika ngazi ya msingi juu mwanafunzi ataonesha ujuzi wa:-

2.1 Kuishi kwa kufuata maagizo ya msingi ya kidini.
2.2 Kujifunza na kutathmini vyanzo vya hekima vinavyopatikana katika dini.
2.3 Kufafanua matukio muhimu katika historia ya Dini ya Kiislamu na mafunzo yake katika maisha ya kila siku.
2.4 Kuishi kwa kufuata maadili na kuwa na ustahamilivu kwa wengine.

## 3.0 MATOKEO MAHSUSI

3.1 Kutekeleza misingi ya kumtegemea Allah (S.W) katika maisha.

3.2 Kutumia mafunzo yanayotokana na Qur-ani na Hadithi katika kutekeleza ibada.

3.3 Kujenga tabia ya kufanya usafi, kutekeleza sala, kutoa zaka, funga na hijja ili kupata radhi za Allah (S.W) na kujipamba na tabia za kiislamu zitakazomuwezesha kuishi vyema na watu waliomzunguka popote atapokua.

3.4 Kupata weledi katika historia ya kiislamu.

3.5 Kufuata tabia na mwenendo wa Mtume Muhammad (S.A.W) katika kusimamia misingi ya dini ya kiislamu.

**MUUNDO WA MTIHANI**

Mtihani wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu utakuwa na sehemu tano (5) ambazo ni A, B, C, D na E na utafanywa kwa muda wa saa mbili na nusu (2:30) na kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu utafanywa kwa muda wa saa tatu (3:00). Mtihani huu utakuwa na jumla ya maswali kumi (10). Watahiniwa watatakiwa kujibu maswali yote kutoka sehemu A, B, C, D na atajibu swali moja (1) kutoka sehemu E. Mtihani huu utakuwa na jumla ya alama 100.

**SEHEMU A:** Itakuwa na alama thelathini (30).

Sehemu hii itakuwa na maswali mawili (1 na 2).

Swali nambari moja (1) litakuwa na vifungu kumi (10) vya maswali ya kuchagua jawabu sahihi (multiple choice items). Kila kifungu kimoja kitakuwa na alama moja (1) na kufanya jumla ya alama 10. Swali hili litahusiana na mada zinazotokana na Qur-ani na Tafsiri pamoja na Sayansi ya Qur-ani.

Swali nambari mbili (2) litahusiana na kutafsiri aya za Qur-ani na kutoa mafunzo ya sura. Swali hili litakuwa na jumla ya alama ishirini (20).

**SEHEMU B:** Itakuwa na alama kumi (10).

Sehemu hii itakuwa na swali moja (1) swali nambari (3).

Swali nambari tatu (3) litahusisha mada ya Tawhidi kwa kujibu ''Kweli'' au ''Sikweli'' litakuwa na vifungu kumi (10) ambapo kila kifungu kitakuwa na alama moja (1). Swali hili litakuwa na jumla ya alama kumi (10).

**SEHEMU C:** Itakuwa na alama ishirini (20).

Sehemu hii itakuwa na maswali mawili (2) swali la (4 na 5).

Swali nambari nne (4) litakuwa ni la kujaza sehemu kumi (10) zilizo wazi kutoka katika mada ya Hadithi za Mtume (S.A.W) na kuleta maana ya maneno yaliyotumika katika Hadithi, kila jawabu litakuwa na alama moja (1). Swali hili litakuwa na jumla ya alama kumi (10).

Swali nambari tano (5) litahusu mada ya Hadithi. Swali hili litakuwa la kutafsiri Hadithi na kutoa mafunzo ya Hadithi. Swali hili litakuwa na alama kumi (10).

**SEHEMU D:** Itakuwa na alama thelathini (30).

Sehemu hii itakuwa na maswali matatu (3), swali nambari (6, 7 na 8). Maswali haya yatakayotokana na mada ya Fiqhi na Malezi. Kila swali litakuwa na alama kumi (10) na kufanya jumla ya alama thelathini (30).

Swali nambari sita (6) litakuwa la kujaza mapengo.
Swali nambari saba (7) litakuwa la kujaza mapengo kwa kuchagua jawabu sahihi.
Swali nambari nane (8) litakuwa la kuelezea kwa urefu.

**SEHEMU E:** Itakuwa na alama kumi (10).

Sehemu hii itakuwa na jumla ya maswali mawili (2), swali nambari (9 na 10). Maswali haya yatakayotokana na mada ya Tarekhe ya Kiislamu. Katika sehemu hii mtahiniwa atatakiwa kujibu swali moja lenye alama kumi (10).

**MADA ZITAKZOTAHINIWA**

1. Qur-ani na tafsiri pamoja na sayansi ya Qur-ani.
2. Hadithi
3. Fiqhi
4. Malezi
5. Tawhidi
6. Historia /Tarekhe

## JADWELI LA KUTAHINI DINI

| | | STADI ZA KUTAHINIWA | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| NAMBA | **MADA KUU** | KUKUMBUKA | UFAHAMU | MATUMIZI | UCHAMBUZI | TATHMINI | UBUNIFU | IDADA YA MASWALI | ASILIMIA YA MASWALI KWA KILA IDADI |
| 1. | QUR-ANI NA TAFSIRI, SAYANSI YA QUR-ANI | | | | | | | 6 | 30.46 |
| 2. | HADITHI | | | | | | | 2 | 10.41 |
| 3. | FIQHI | | | | | | | 6 | 29.16 |
| 4. | TAWHIDI/ IMANI | | | | | | | 2 | 9.89 |
| 5. | HISTORIA / TAREKHE | | | | | | | 3 | 12.76 |
| 6. | MALEZI | | | | | | | 2 | 7.29 |
| | IDADI YA MASWALI | | | | | | | 21 | |
| | ASILIMIA YA MASWALI KWA KILA STADI | | | | | | | | 100% |